- Watumishi wapatao 45 wameajiriwa kwa mwaka 2020/2021 katika idara za Elimu Msingi, Sekondari, Afya, Utawala na Ujenzi.
- Vikao vya kisheria 24 vimefanyika katika ngazi ya Halmashauri
- Malipo ya stahiki za watumishi 67 yamefanyika kulingana na kanuni, taratibu na sheria

#### **(h) Halmashauri ya Wilaya ya Bukoba**

- Ujenzi wa Jengo la Ofisi ya Makao Makuu ya Halmashauri katika eneo la Bujunangoma awamu ya kwanza na ya pili (shilingi 2,000,000,000.00)
- Ujenzi wa wodi mbili za wanaume na wanawake, jengo la upasuaji na jengo la kuhi-fadhia maiti katika hospitali ya Wilaya Bujunangoma (shilingi 800,000,000.00)
- Ukamilishaji wa zahanati 3 za Mugajwale, Kazinga na Bituntu (shilingi 150,000,000.00)
- Ujenzi wa vyumba tisa vya madarasa katika shule za msingi Mashule B, Kyampisi, Karonge, Kyamuolaile, Ruhoko, Rutete, Ruhunga, Kamuzora na Umoja (shilingi 112,500,000.00)
- Ukamilishaji wa vyumba 6 vya maabara kwa shule za sekondari za Izimbya, Kabale, Katale, Kyamuolaile, Ruhunga na Mwemege (shilingi 150,000,000.00)
- Uboreshaji wa kituo cha afya Rubale (shilingi 250,000,000.00)
- Ujenzi wa nyumba ya watumishi (3 in one) katika hospitali ya Wilaya Bujunangoma (shilingi 90,000,000.00)
- Ujenzi wa shule mpya ya sekondari Rukoma (shilingi 470,000,000.00)



Piicha ya Jengo la Ofisi ya Halmashauri ya Wilaya ya bukoba

### **Taarifa ya Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo kupitia Fedha za Mapato ya Ndani ya Halmashauri**

Katika mwaka wa fedha 2021/2022 hadi kufikia mwezi Februari, 2022 Halmashauri za Mkoa wa Kagera zimetoa kiasi cha **Tshs 6,961,664,341.71** katika kutekeleza shughuli za maendeleo sawa na asilimia **106** ya kiasi chote kilichotakiwa kutolewa kwa ajili ya miradi katika kipindi hicho kulingana na makusanyo halisi ya asilimia 40 (**Tshs 6,569,200,517.80**).

**Jedwali Na. 8. Jedwali la Miradi Iliyotekezwa kwa asilimia 40 ya Mapato ya ndani**

Na	Hal-mashauri	Kazi zilizopangwa	Idadi ya Miradi	Bajeti iliyoidhinishwa	Kazi Zilizotekezwa	Kiasi cha Fedha kili-chotolewa	Asilimia ya Fedha Zilizoto	Maoni
<b>A</b>	<b>Miradi iliyolekwa ya Sekta ya Afya na Elimu</b>							
		Ukamilishaji ujenzi wa Zahanati	3	150,000,000	Ujenzi hanamu, upauaji, urekebishaji kuta	130,000,000	86.7	H a t u a ukamilishaji
	Biharamulo DC	Ukamilishaji vyumba 17 vya madarasa na vyoo matundu 16 shule za msingi 13	17	137,500,000	Ukamilishaji vyumba 25 vya madarasa na matundu ya vyoo 10 shule za msingi 7 ujenzi unaendelea	195,795,123	142.4	Ujenzi un-aendelea
		Ukamilishaji wa ma-boma Madarasa 13 shule 4 za sekondari	13	137,500,000	Ukamilishaji wa vyumba 3 shule 2 za sekondari umekamilika	11,300,000	8.22	Ujenzi umekamilika
		<b>Jumla Ndogo</b>		<b>425,000,000.00</b>		<b>337,095,123.00</b>	<b>79.32</b>	
<b>B</b>	<b>Miradi mingine iliyotekezwa na fedha za mapato ya ndani ya Halmashauri</b>							
		Kutoa mikopo kwa vi-kundi vya wanawake 16, vijana 16 na wenye ulemavu 8	40	171,162,373.00	Kutoa mikopo	136,143,906.00	66.7	
	Biharamulo DC	Ufuatiliaji na tathimini ya miradi		55,000,000.00	Kufanya ufuatiliaji na tathimini ya utekelezaji wa miradi	47,708,366	86.7	
		Utekelezaji wa shughuli za lische kulingana na mkataba wake	-	33,937,119	Shughuli za lische kulingana na mkataba zime-tekelezwa	22,628,230	66.7	Utekelezaji un-aendelea
		Kusaidia ukamilishaji (kuezeka ) Ofisi ya Kijiji cha Nyamigogo	1	0	Kupaua jengo la ofisi ya Kijiji cha Nyamigogo	1,000,000	100	Upauaji wa jengo umekamilika
		<b>Jumla Ndogo</b>		<b>259,649,492.00</b>		<b>207,480,502.00</b>		
		<b>Jumla Biharamulo DC</b>		<b>684,649,492.00</b>		<b>541,755,594.96</b>		

Na	Hal-mashauri	Kazi zilizopangwa	Idadi ya Miradi	Bajeti Iliyoidhinishwa	Kazi Zilizotekelezwa	Kiasi cha Fedha kili-chotolewa	Asilimia ya Fedha Zilizotolewa	Maoni
		Ujenzi wa kituo cha afya Kashai	1	500,000,000.00	Ujenzi wa kituo cha afya	286,135,488.64		
	Bukoba MC				Ukamilishaji zahanati Buhembe	20,000,000.00		
					Ujenzi wa jengo la x-ray kituo cha afya Zamzam	15,371,000.00		
					Ujenzi zahanati Kibeta	20,000,000.00		
					Ujenzi vyumba 18 vya madarasa	50,000,000.00		
					Ukarabati vyoo matundu 22 Kashai sekondari	14,700,000.00		
					Ujenzi vyumba 18 vya madarasa	38,685,959.79		
					Ukamilishaji ujenzi vyoo Nyanga sekondari	900,000.00		
		<b>Jumla Ndogo</b>		<b>500,000,000.00</b>		<b>445,792,448.43</b>		
<b>B</b>	<b>Miradi mingeni iliyotekelezwa na fedha za mapato ya ndani ya Halmashauri</b>							
		Kutoa mikopo kwa wanawake vijana na watu wenye ulemavu		222,000,000	Vikundi 13 vimepatiwa mkopo (6 wanawake, 4 vijana na 3 watu wenye ulemavu)	153,597,482.81	58.2	
	Bukoba MC				Matengenezo ya bara-bara kahororo – kyaya 5,000,000	5,000,000.00		
					Kulipa ndeni la TIB 10,000,000	10,000,000.00		
		<b>Jumla Bukoba MC</b>		<b>722,000,000</b>		<b>614,389,931.24</b>		

Na	Hal-mashauri	Kazi zilizopangwa	Idadi ya Miradi	Bajeti Iliyoidhinishwa	Kazi Zilizotekelezwa	Kiasi cha Fedha kili-chotolewa	Asilimia ya Fedha Zilizoto	Maoni
<b>A</b>	<b>Miradi iliyolekezwa ya Sekta ya Afya na Elimu</b>							
		Kuchangia ujenzi wa Madarasa 3 na Ofisi ndogo ya walimu katika shule mpya ya Msingi Miillo	1	50,000,000.00	Uchangiaji upatikanaji wa vifaa vya viwandani	25,000,000	50	Madarasa 3 yamekamiliika na Ofisi ndogo ya walimu
	Karagwe	Kuchangia ukamilishaji wa Vyoo katika Shule za Msingi za Rumanyika, Ihanda, Suzana na Karagwe	7	34,682,200.00	Kuchangia nguvu za wananchi kwa upatikanaji vifaa vya viwandani	32,000,000	94	Vyoo matundu 16 yamekamiliika
		Ujenzi wa madarasa Nyakabila	1	0	Ukamilishaji	10,000,000	100	Ukamilishaji
		Kuchangia ujenzi wa matundu ya vyoo katika shule za Msingi na sekondari za Chabuhora, Kagutu, na Igurwa Sekondari	4	54,559,702.00	Kuchangia nguvu za wananchi kwa upatikanaji vifaa vya viwandani	52,527,522.30	96	Vyoo matundu 24 yamekamiliika
		Ukamilishaji ujenzi wa Mabweni katika Shule ya Sekondari Ruhinda	1	80,000,000.00	Ukamilishaji	25,000,000	31	Ujenzi unaendelea
		Kuchangia ujenzi wa Miundombinu kwenye shule za Sekondari 3 mpya za Bashungwa, Kigarama, na Bushangaro (@ Shs.12,500,000)	3	37,500,000.00	Uchangiaji upatikanaji wa vifaa vya viwandani	71,254,367.70	190	Ujenzi unaendelea
		Ujenzi wa madarasa Bugene na Bujuruga Sekondari	2	0	Kuchangia nguvu za wananchi kwa upatikanaji vifaa vya viwandani	65,000,000	100	Ujenzi unaendelea
		Ukamilishaji ujenzi wa Wodi 3 Hospitali ya wilaya	3	40,000,000	Ujenzi unaendelea	40,000,000	100	Kazi inaendelea
		Kuchangia ujenzi Zahanati Rukole		50,000,000.00	Upandishaji kuta	25,000,000.00	50	Upandishaji kuta
		Kuchangia ujenzi Zahanati Chabalisa		50,000,000.00	Upandishaji kuta	25,000,000.00		Upandishaji kuta
		Kuchangia Ujenzi wa Zahanati		0	Ujenzi vyoo	8,000,000	100	Ujenzi vyoo
		<b>Jumla Ndogo</b>		<b>396,741,902.00</b>		<b>378,781,890.00</b>		



Na	Hal-mashauri	Kazi zilizopangwa	Idadi ya Miradi	Bajeti Iliyoidhinishwa	Kazi Zilizotekelezwa	Kiasi cha Fedha Kili-chotolewa	Asilimia ya Fedha Zilizozilizo	Maoni
<b>B</b>	<b>Miradi mingeni iliyotekelezwa na fedha za mapato ya ndani ya Halmashauri</b>							
		Mikopo vikundi vya wanawake, vijana na wenye ulemavu		267,190,400.00	Mikopo imetolewa kwa vikundi	209,327,129.47	78	Mikopo ime-tolewa kwa vi-kundi
		Kudhibiti UKIMWI na watoto walio katika mazingira hatarishi		5,000,000.00	Kuwezesha huduma za kujikimu	5,000,000	100	Kuwezesha huduma za kuji-kimu
	Karagwe	Uendeshaji wa chanjo dhidi ya magonjwa yafuatayo BQ, CBPP, FMD and Rabies		160,000,000.00	Kudhibiti majongwa ya mifugo	91,023,157.74	57	Kudhibiti majongwa ya mifugo
		Ujenzi wa Uzio katika eneo la mnada wa Nyai-shozi		15,000,000.00	Ujenzi wa ukuta	14,132,308.41	94	Ujenzi wa ukuta
		Ununuzi Miche ya kahawa	200,000	40,000,000	Miche imegawiwa kwa wakulima	20,000,000	50	Kazi inaendelea
		Kufanya ukaguzi wa taarifa za fedha na shughuli za vyama vya ushirika vya akiba na mikopo kumi na nne (14) na vyama vya ushirika vya msingi hamsini na sita (56) kufikia mwezi Juni 2022		1,000,000.00	Ukaguzi unaendelea	1,000,000.00	100	Ukaguzi unaendelea
		Ukarabati wa majengo ya Halmashauri		15,000,000.00	Upakaji rangi na kubandika vigaa	11,000,000.00	73	Upakaji rangi na kubandika vigaa
		Kuchangia shughuli za ustawi wa jamii		5,000,000.00	Kuwezesha huduma za kujikimu	5,000,000.00	100	Kuwezesha huduma za kujikimu
		Kuwezesha Huduma za lische kwa watoto chini ya miaka 5		80,765,000.00	Huduma za lische zimetolewa	56,000,000.00	69	Huduma za lische zimetolewa
		Kugharimia upatikanaji wa hati za maeneo yenye miradi ya <b>kimkakati ya mapato</b> na kuaimisha majina ya mitaa <b>Anuani</b>		22,500,000.00	Hati za eneo la Hospitali ya wilaya imepatikana	10,000,000.00	44	Hati za eneo la Hospitali ya wilaya imepatikana

Na	Hal-mashauri	Kazi zilizopangwa	Idadi ya Miradi	Bajeti Iliyoidhinishwa	Kazi Zilizotekelezwa	Kiasi cha Fedha Kili-chotolewa	Asilimia ya Fedha Zilizozilizo	Maoni
		Kuwezesha Ujenzi wa Mfereji wa maji ya Mvua (water storm drainage)		10,000,000.00	Mfereji umejengwa	10,000,000.00	100	Mfereji umejengwa
		Kuchangia Ujenzi wa Ofisi za Vijiji Rugu na Rukale ifikapo Juni 2022		15,000,000.00	Ujauaji kuta	15,000,000.00	100	Ujauaji kuta
		Miradi ngazi ya Vijiji na Kata		0	Miradi imewezesha	68,000,000	100	Miradi imewezesha
		Uendelezaji wa ujenzi wa Uwanja wa Michezo wa <b>Bashungwa</b> kwa njia ya Ubia - <i>Public Private Partnership</i> – <b>PPP ( Kuandaa Documents na mawasiliano na wa-</b>		25,000,000.00	Ujenzi unaendelea	10,000,000.00	40	Ujenzi unaendelea
		Kufanya ujenzi wa soko La Kayanga kwa njia ya Ubia Public Private Partnership – <b>PPP ( Kuandaa Documents na mawasiliano</b>		1,000,000.00	Michoro inaendelea kuandaliwa	1,000,000.00	100	Michoro inaendelea kuandaliwa
		Uendelezaji wa stendi mpya ya Kayanga kwa kuandaa Michoro, <b>Design</b> na kukamilisha maandiko		14,000,000.00	Michoro inaendelea kuandaliwa	2,000,000.00	14	Michoro inaendelea kuandaliwa
		<b>Jumla Ndogo</b>		<b>675,455,400.00</b>		<b>527,482,595.62</b>		
		<b>Jumla Karagwe DC</b>		<b>1,072,197,302.00</b>		<b>907,264,485.62</b>		

A Miradi iliyolekezwa ya Sekta ya Afya na Elimu								
	Kyerwa DC	Ujenzi wa Kituo vya Afya Mabira	1	500,000,000	Ujenzi OPD-Jengo la wagonjwa wa nje, Maa-bara, Wodi ya wazazi (Marternity ward), Ujenzi upo hatua ya kuzeka	400,000,000	80	
		<b>Jumla Ndogo</b>		<b>500,000,000</b>		<b>400,000,000</b>	<b>80</b>	

Na	Hal-mashauri	Kazi zilizopangwa	Idadi ya Miradi	Bajeti Iliyoidhinishwa	Kazi Zilizotekelezwa	Kiasi cha Fedha Kili-chotolewa	Asilimia ya Fedha Zilizozidhinishwa	Maoni
<b>B</b>	<b>Miradi mingine iliyotekelezwa na fedha za mapato ya ndani ya Halmashauri</b>							
	Kyerwa DC	Ukarabati wa mnada wa mazao ya mifugo Katera.	1	8,075,000.00	Ununuzi wa vifaa vya viwandani na kufanya ukarabati.	8,075,000.00	100	Mradi aendelea
		Ujenzi wa matundu 6 ya vyoo katika mnada wa muda wa Murongo.	6	0.00	Kujenga msingi, kuta, kuezeka na kufanya ufuatiliaji.	7,000,000.00	100	Mradi aendelea
		Ununuzi na usambazaji wa miche ya Kahawa 54,666 na viriba kwa wakulima kata 24.	1	10,200,050.00	Ununuzi na usambazaji wa miche kwa wakulima wa kata zote 24.	11,864,910.00	116	Miche imelipiwa
		Ukarabati wa kituo cha kutolea huduma za ugani Katera.	1	10,717,808.00	Kununua vifaa na kufanya ukarabati.	10,000,000.00	93	Mradi umekamiliika
		Ujenzi wa matundu 10 ya vyoo katika Stendi ya Nkwenda Maziwa	10	20,099,950.00	Ununuzi wa vifaa, kujenga msingi, kuta, kuezeka na kufanya ukamilishaji	20,099,950.00	100	Mradi umekamiliika
		Ukamilishaji wa nyumba 2 (2in1) za watumishi Rwenkorongo	2	25,000,000.00	Kupiga lipu, rangi na kufanya ukamilishaji	25,028,000.00	100	Mradi umekamiliika
		Kuwezesha utoaji wa mikopo ya 10%, 4% kwa vijana, 4% kwa Wanawake na 2% kwa watu wenye ulemavu.	1	199,885,336.00	Utoaji wa mikopo ya vikiundi	206,141,589.27	103	Mikopo ime-tolewa
		Kufanya shughuri za usimamizi na ufatiliaji wa miradi katika kata 24.	1	18,738,200.00	Kufanya usimamizi wa miradi kata Kata 24	10,825,000.00	58	Usimamizi wa miradi aendelea
		Mafunzo ya O & OD kwa ajili maandalizi ya Mpango na bajet mwaka wa fedha 22.23	1	0.00	Kufanya mafunzo ya O & OD kwa watumishi	9,464,000.00	100	Mafunzo yame-fanyika kwa waweshaji 82 wa ngazi ya Kata

Na	Hal-mashauri	Kazi zilizopangwa	Idadi ya Miradi	Bajeti Iliyoidhinishwa	Kazi Zilizotekelezwa	Kiasi cha Fedha kilichotolewa	Asilimia ya Fedha Zilizozilizo	Maoni
		Ukarabati wa nyumba ya Mkurugenzi	1	0.00	Kununua vifaa vya viwandani na kupiga rangi	4,675,500.00	100	Ukarabati umekamilika
		Ununuzi wa magari mawili (2) TOYOTA PICK UP double cabin na gharama za bima gari la Mkurugenzi SM 14067	2	0.00	Kulipia ununuzi wa magari 2	191,393,024.63	100	M a g a r i yamenunuliwa
		Kuunganisha maji kwenye eneo la ujenzi wa shule mpya Rubwera	1	0.00	Kununua vifaa na kuunganisha maji	8,532,800.00	100	M r a d i umekamilika
		Utengenezaji wa Vitanda (Double decker 66, single 01) katika shule ya Sekondari Mabira	66	0.00	Kutengeneza vitanda 66	15,280,000.00	100	V i t a n d a v i m e t e n n a genezwa na vinatumika
		Ujenzi wa stoo na vyoo vya muda katika shule mpya Rubwera	1	0.00	Kununua vifaa na ku-fanya vya ujenzi na kujenga stoo	4,054,000.00	100	M r a d i umekamilika
		Ukusanyaji wa takwimu za masuala ya lische katika Kata	24	0.00	Kukusanya takwimu	15,882,856.30	100	Takwimu zimekusanywa
		<b>Jumla ndogo</b>		<b>299,541,344.00</b>		<b>548,316,630.20</b>		
		<b>Jumla Kyerwa DC</b>		<b>799,541,344.00</b>		<b>948,316,629.30</b>		
<b>A</b>	<b>Miradi iliyolekezwa ya Sekta ya Afya na Elimu</b>							
	Missenyi DC	Ukamilishaji wa vyumba 6 vya madarasa Elimu Msingi	6	64,471,006.00	umekamilika	64,471,006.00	93	Miradi ipo hatua ya ukamilishaji
		Ukamilishaji wa vyumba 3 vya maabara	3	14,000,000.00	vimekamilika	14,000,000	100	
		Ujenzi wa matundu 31 ya vyoo katika shule 6 za msingi	6	53,300,000.00	yamekamilika	53,300,000.00	100	

Na	Hal-mashauri	Kazi zilizopangwa	Idadi ya Miradi	Bajeti Iliyoidhinishwa	Kazi Zilizotekelezwa	Kiasi cha Fedha kilichotolewa	Asilimia ya Fedha Zilizozilizo	Maoni
		Ukamiliishaji zahanati 3	3	25,589,340.00	Hatua ya ukamilishaji	25,589,340.00	95	
		Ujenzi wa kituo cha afya Kakunyu	1	500,000,000.00	Ujenzi wa maabara na OPD hatua ya ukamilishaji na RCH na maternity hatua ya msingi	500,000,000.00	100	
		<b>Jumla Ndogo</b>		<b>657,360,346.00</b>		<b>657,360,346.00</b>		
<b>B</b>	<b>Miradi mingeni iliyotekelezwa na fedha za mapato ya ndani ya Halmashauri</b>							
	Missenyi DC	Kupunguza udumavu kwa watoto chini ya ya miezi 36		43,000,000.00	Kupunguza udumavu kwa watoto chini ya ya miezi 36	30,811,665.45	80	Kazi zinaendelea
		Kuwezesha uzalishaji wa Mazao ya kilimo kwa wakulima kwa kuwapatia viaadu na Mbegu bora za uzalishaji katika	11	45,000,000.00		45,000,000.00	100	Kazi zinaendelea
		Kuwezesha utekelezaji wa shughuli za Mifugo na uvuvi kwa kutoa chanjo ya mifugo na uboreshaji wa shughuli za uvuvi	5	40,000,000.00	Kuwezesha utekelezaji wa shughuli za Mifugo na uvuvi kwa kutoa chanjo ya mifugo na uboreshaji wa shughuli za uvuvi	23,400,000.00	59	Kazi zinaendelea
		Kuwezesha utekelezaji wa shughuli za Ardhi na Maliasili kwa kulipa fidia eneo kwa ajili ya maege- gesho ya matori Mutukula	3	88,124,000.00	Kuwezesha utekelezaji wa shughuli za Ardhi na Maliasili kwa kulipa fidia eneo kwa ajili ya maege- sho ya matori Mutukula	88,124,000.00	100	Kazi zinaendelea
		Kuwezesha ujenzi wa miundombinu kwenye stendi ya Kyaka, ujenzi wa barabara za mitaa Kyaka na ukarabati wa miundombinu kwenye stendi ya Mutukula	3	40,874,000.00	Kuwezesha ujenzi wa miundombinu kwenye stendi ya Kyaka, ujenzi wa barabara za mitaa Kyaka na ukarabati wa miundombinu kwenye stendi ya Mutukula	40,874,000.00	100	Kazi imekamilika

Na	Hal-mashauri	Kazi zilizopangwa	Idadi ya Miradi	Bajeti Iliyoidhinishwa	Kazi Zilizotekelezwa	Kiasi cha Fedha kilichotolewa	Asilimia ya Fedha Zilizozilizo	Maoni
		Kuwezesha na kutoa mikopo isiyo na liba kwa vikundi 100 vya kiu-chumi kwa vijana	16	308,387,080.00	Kuwezesha na kutoa mikopo isiyo na liba kwa vikundi vya kiuchumi kwa vijana	292,600,943.52	95	Vikundi 50 vimepatiwa mikopo (wanawake 29, vijana 13 na wenye ulemavu 8)
		<b>Jumla Ndogo</b>		<b>569,385,080.00</b>		<b>527,498,049.29</b>		
		<b>Jumla Misenyi DC</b>		<b>1,221,585,040.00</b>		<b>1,231,599,962.78</b>		
<b>A</b>	<b>Miradi iliyolekezwa ya Sekta ya Afya na Elimu</b>							
		Ujenzi wa Zahanati	2	100,000,000.00	Ujenzi wa Zahanati za Kablanzwili na Kigina	100,000,000.00	100	Ujenzi upo hatua ya umal-izilaji
	Ngara DC	Ukamilishaji wa ma-boma Madarasa	2	40,000,000.00	Ujenzi wa vyumba vya madarasa katika Shule ya Sekondari Ngara High	40,000,000.00	100	Ujenzi umekamilika
		<b>Jumla Ndogo</b>		<b>140,000,000.00</b>		<b>140,000,000.00</b>		
<b>B</b>	<b>Miradi mingeni iliyotekelezwa na fedha za mapato ya ndani ya Halmashauri</b>							
	Ngara DC		68	40,000,000.00	Ununuzi wa POS 68	40,000,000.00	100	
			2	134,644,776.00	Ujenzi wa Maegesho ya Nzaza na Benaco	134,644,776.00	100	
			1	22,000,000.00	Ununuzi wa Eneo la kum-waga taka Ngumu (Dampo)	22,000,000.00	100	
			1	20,000,000.00	Ukarabati wa Rest house	20,000,000.00	100	
			1	30,345,973.00	Ununuzi wa kifaa vya	30,345,973.00	100	
			1	7,000,000.00	Ununzi wa mbolea uandaaji wa kitalu cha michikichi	7,000,000.00	100	
			1	10,000,000.00	Uanzishwaji wa kitalu cha miche ya kahawa	10,000,000.00	100	

Na	Hal-mashauri	Kazi zilizopangwa	Idadi ya Miradi	Bajeti Iliyoidhinishwa	Kazi Zilizotekelezwa	Kiasi cha Fedha Kili-chotolewa	Asilimia ya Fedha Zilizozilizo	Maoni
			1	5,000,000	Uandaaji wa kitalu cha	5,000,000.00	100	
			1	5,000,000	Kununua mbegu bora za alizeti	5,000,000.00	100	
			1	30,000,000	Uchangiaji wa Afua za Lishe	21,391,000.00		
			2	33,800,000	Ujenzi wa Matundu 26 ya vyoo katika Shule 2 Sekondari za Lukole na Ngara	33,800,000.00		
				184,990,000.00	Uchangiaji wa mfuko wa wanawake, vijana na wale-mavu 10%	197,864,991.70	106.9	
			105	116,000,000.00	Ujenzi wa Matundu ya vyoo 105 katika Shule za msingi	116,000,000.00	100	
			1	12,000,000.00	Ununuzi wa vifaa vya ujenzi shule ya Msingi Muganza	12,000,000.00	100	
			1	11,000,000	Ununuzi wa vifaa vya ujenzi shule ya Msingi Nyamiaga	11,000,000.00	100	
			1	37,000,000.00	Ufuatiliaji na Tathmini ya Miradi	13,650,000.00		
				<b>688,780,749.00</b>		<b>679,696,740.00</b>		
				<b>828,780,749.00</b>		<b>819,696,740.70</b>		
<b>A Miradi iliyolekezwa ya Sekta ya Afya na Elimu</b>								
	Muleba DC	Ujenzi kituo cha afya	1	500,000,000	Ujenzi kituo cha afya	455,000,000	91%	
		<b>Jumla Ndogo</b>		<b>500,000,000</b>		<b>455,000,000</b>		
<b>B Miradi mingeni iliyotekelezwa na fedha za mapato ya ndani ya Halmashauri</b>								
	Muleba DC	Kutoa mikopo nafuu kwa makundi maalum ya Wanawak, vijana na		297,747,761.00	kutoa mikopo nafuu kwa makundi maalum ya Wanawake, vijana na	297,747,761.00	100	

Na	Hal-mashauri	Kazi zilizopangwa	Idadi ya Miradi	Bajeti Iliyoidhinishwa	Kazi Zilizotekelezwa	Kiasi cha Fedha kilichotolewa	Asilimia ya Fedha Zilizotolewa	Maoni
		Ujenzi wa ghati - Goziba	1	25,257,655.20	ujenzi wa ghati - Goziba	25,257,655.20	100.0	
		Ukarabati wa majosho	20		ukarabati wa majosho		100.0	
		Ujenzi wa choo cha	6		Ujenzi wa choo cha		100.0	
		Kuchangia gharama za usambazaji wa miche ya parachichi, mihogo, vi-	4	1,745,000.00	Kuchangia gharama za usambazaji wa miche ya parachichi,	1,745,000	100.0	
		Ujenzi wa Ghati kimoyomoyo	1	36,000,000.00	Ujenzi wa Ghati kimoyomoyo	36,000,000.00	100.0	
		Ujenzi wa Ghati Kerebe	1	28,000,000.00	Ujenzi wa Ghati Kerebe	28,000,000.00	100.0	
		Ukamilishaji wa ofisi ya	1		ukamilishaji wa ofisi		100.0	
		Utawala		6,273,500.00		6,273,500	98%	
		<b>Jumla Ndogo</b>		<b>1,283,459,893.50</b>		<b>1,031,403,072.07</b>		
		<b>Jumla Muleba DC</b>		<b>1,783,459,893.50</b>		<b>1,486,403,072.07</b>		

**A Miradi iliyolekezwa ya Elimu na Afya**

		Ujenzi wa Zahanati Mulahya	1	100,000,000.00	Kuinua kuta na ku-paua	50,000,000.00	50	-
	Bukoba DC	Ukamilishaji wa ujenzi wa vyumba vya mada-rasa, shule za msingi Kanazi B, Kilimile B, Kaishaza na Kamuli	4	47,500,000.00	Ukamilishaji wa madarasa	47,500,000.00	100	-
		Ukamilishaji wa ujenzi wa vyumba vya mada-rasa, shule ya sekondari Rukoma	2	25,000,000.00	Ukamilishaji wa da-rasa	25,000,000.00	100	-
		<b>Jumla Ndogo</b>		<b>175,000,000.00</b>		<b>122,500,000.00</b>	<b>70</b>	



Na	Hal-mashauri	Kazi zilizopangwa	Idadi ya Miradi	Bajeti Iliyoidhinishwa	Kazi Zilizotekelezwa	Kiasi cha Fedha kilichotolewa	Asilimia ya Fedha Zilizotolewa	Maoni
<b>B</b>	<b>Miradi mingeni iliyotekelezwa na fedha za mapato ya ndani ya Halmashauri</b>							
	B u k o b a DC	Uchangiaji wa asilimia 10 za Wanawake, Vijana na Watu wenye Ulemavu	1	144,200,000	Utoaji wa Mikopo	103,100,000	71.5	-
		Lishe kwa watoto chini ya miaka mitano	1	75,000,000	Utoaji wa lishe kwa watoto chini ya miaka 5	40,190,000	54	-
		Ujenzi wa uzio wa mnada Nshehe	1	12,400,000	Ujenzi wa uzio umekamilika	12,400,000	100	-
		10,000,000	1	15,000,000	Usambazaji wa miche katika Kata 29	15,000,000	100	-
		20,000,000	1	10,000,000	Utoaji wa chanjo	10,000,000	100	-
		Ujenzi wa matundu 10 ya vyoo katika shule ya sekondari Kashozi	1	20,000,000	Ujenzi wa vyoo umekamilika	20,000,000	100	-
		Ujenzi wa choo katika Kijiji cha Buguruka	1	5,000,000	Ujenzi wa choo un-aendelea	5,000,000	100	-
		Usimamizi wa miradi	1	62,200,000	Usimamizi umefanyika	13,159,000	21	-
		Ukarabati wa mitambo (boti 10,000,000 na grader 10,500,000)	2	20,500,000	Ukarabati umekamilika.	20,500,000	100	-
		Ujenzi wa choo matundu 4 katika mwalo wa Karwazi.	1	8,597,000	Ujenzi wa uko katika hatua ya utekelezaji.	8,597,000	100	-
		Ununuzi wa POS	1	7,310,000	POS zimenunuliwa.	7,310,000	100	-
		<b>Jumla Ndogo</b>		<b>380,207,000.00</b>		<b>255,256,000.00</b>		
		<b>Jumla Bukoba DC</b>		<b>555,20707,000.00</b>		<b>409,417,895.00</b>		
		<b>Jumla Mkoa</b>		<b>6,569,200,517.80</b>		<b>6,961,664,341.71</b>		

## Taarifa za Mikopo ya Asilimia 10 ya Mapato ya Ndani ya Halmashauri

Katika mwaka 2021/2022 hadi kufikia mwezi Februari, 2022 Halmashauri za mkoa wa Kagera zimetoa kiasi cha **Tshs 1,611,092,682.93** sawa na asilimia **101** Kwa vikundi **365** vya wanawake, vijana na watu wenye ulemavu. Ambapo katika kiasi hicho, wanawake wamepata **Tshs 763,604,467.67**, vijana **Tshs 681,577,423.00** na watu wenye ulemavu **Tshs. 165,910,792.20**

## Jedwali Na. 9 Mchanganuo kwa makundi ya Wanawake, Vijana na Watu wenye Ulemavu kwa uwiano wa 4-4-2 hadi Februari, 2022

Na	Halmashauri	Mapato yasiyo-lindwa	Asilimia 10	Kiasi kilichopelekwa	Fedha iliyotolewa kwenye vikundi hadi Februari 2022				Idadi ya Vikundi		
					Wanawake - 4	Vijana - 4	Watu Wenye Ulemavu - 2	Wanawake	Vijana	Watu Wenye Ulemavu	
1	Biharamulo DC	1,354,388,980.00	135,438,898.00	136,143,906.29	83,500,000.00	45,643,906.29	7,000,000.00	17	11	4	
2	Bukoba DC	1,023,544,737.50	102,354,473.75	103,100,000.00	40,000,000.00	53,100,000.00	10,000,000.00	12	21	2	
3	Bukoba MC	1,535,974,828.10	153,597,482.81	153,597,482.81	77,000,000.00	65,597,482.81	11,000,000.00	6	4	3	
4	Karagwe	2,184,222,570.00	218,422,257.00	227,000,000.00	111,980,468.00	84,937,500.00	30,082,032.00	21	11	10	
5	Kyerwa DC	2,041,415,892.70	204,141,589.27	204,141,589.27	95,641,589.27	105,500,000.00	3,000,000.00	20	14	36	
6	Missenyi DC	2,926,009,435.00	292,600,943.50	292,600,943.50	145,226,906.00	139,374,037.50	8,000,000.00	23	12	4	
7	Ngara DC	1,967,000,000.00	196,700,000.00	196,700,000.00	91,132,000.00	68,300,992.00	37,267,008.00	15	8	6	
8	Muleba DC	2,978,827,310.00	297,882,731.00	297,808,761.06	119,123,504.40	119,123,504.40	59,561,752.20	84	11	10	
<b>Jumla Mkoa</b>		<b>16,011,383,753.30</b>	<b>1,601,138,375.33</b>	<b>1,611,092,682.93</b>	<b>763,604,467.67</b>	<b>681,577,423.00</b>	<b>165,910,792.20</b>	<b>198</b>	<b>92</b>	<b>75</b>	

## Taarifa ya Marejesho ya fedha za Mikopo ya Asilimia 10 ya Wanawake, Vijana na Walemavu

Katika kipindi cha kuanzia mwaka 2018/19 hadi Februari 2021/22 Halmashauri za Mkoa wa Kagera zimeweza kutoa Mikopo yenye thamani ya shilingi **Tshs 9,018,044,211.00** kwa vikundi vya Vijana, Wanawake na Watu wenye Ulemavu. Kati ya Fedha hizo kiasi cha fedha zilizorejeshwa ni **Tshs 4,262,207,740.00**. Fedha hizo zimetumika katika kutoa Mikopo kwa Vikundi vya Wanawake, Vijana na Watu wenye Ulemavu **Tshs 3,255,907,374.00** ambapo Wanawake ni **Tshs 2,072,767,173.00**, Vijana **Tshs 1,042,566,038** na watu wenye ulemavu **Tshs 140,574,163.00** Mchanganuo wa Marejesho kwa kila mwaka na kila Halmashauri umeoneshwa katika Jedwali linalofuata; -

### Jedwali Na. 10 Mchanganuo wa Marejesho kwa kila mwaka na kila Halmashauri

Na	Halmashauri	Kiasi cha fedha ambacho kimekopeshwa kuanzia Julai, 2018 hadi Februari, 2022	Kiasi cha fedha ambacho kimerorejeshwa kuanzia Julai, 2018 hadi Februari, 2022	Kiasi kilichokopesha kupitia fedha za Marejesho kuanzia Julai, 2018 hadi Febrauri 2022			Idadi ya Vikundi vilivyokopeshwa kwa fedha za marejesho kuanzia Julai, 2018 hadi Februari, 2022		
				Wanawake - 4	Vijana - 4	Watu Wenye Ulemavu - 2	Wana wake	Vijana	Wenye Ulemavu
1	Biharamulo DC	768,449,529.00	319,475,400.00	229,799,529.00	40,700,000.00	2,000,000.00	55	7	1
2	Bukoba DC	664,380,000.00	293,404,100.00	130,403,000.00	144,147,100.00	18,854,000.00	53	36	6
3	Bukoba MC	1,084,914,000.00	503,920,350.00	360,000,000.00	130,644,000.00	-	79	20	0
4	Karagwe	1,367,313,000.00	859,792,100.00	308,429,000.00	204,210,000.00	31,000,000.00	128	69	12
5	Kyerwa DC	663,228,446.00	134,575,100.00	29,804,622.00	29,804,622.00	14,902,311.00	6	4	4
6	Missenyi DC	1,442,192,151.00	691,115,515.00	199,259,980.00	182,059,371.00	-	49	24	0
7	Ngara DC	623,000,000.00	243,047,893.00	116,000,000.00	56,800,000.00	31,396,000.00	8	3	2
8	Muleba DC	2,404,567,085.00	1,216,877,282.00	699,071,042.00	254,200,945.00	42,421,852.00	243	22	10
<b>Jumla Mkoa</b>		<b>9,018,044,211.00</b>	<b>4,262,207,740.00</b>	<b>2,072,767,173.00</b>	<b>1,042,566,038.00</b>	<b>140,574,163.00</b>	<b>621</b>	<b>185</b>	<b>35</b>

## 2.5 Mafanikio, Changamoto na Mikakati Katika Utekelezaji wa Mipango na Bajeti

### 2.5.1 Mafanikio

- Ufanisi katika ukusanyaji mapato, Halmashauri zimeweza kukusanya mapato kwa asilimia 75 hadi mwezi Februari, 2022 na kati ya mapato hayo halisi (yasiyofungiwa) asilimia 40 imepelekwa kutekeleza shughuli za maendeleo na asilimia 10 katika kuwapa mikopo vikundi vya wanawake, vijana na wenye ulemavu.
- Kuwezesha ukamilishaji wa miundombinu ya vyumba vya madarasa na zahanati 2 kupitia fedha za mapato ya ndani
- Kuwezesha kufanyika kwa vikao vya kisheria vya Halmashauri ikiwa ni kuimarisha utawala bora.
- Madeni ya wazabuni ya muda mrefu yamelipwa hasa wazabuni wa chakula katika shule za sekondari.
- Mafanikio yamekuwepo katika utekelezaji wa miradi ya maendeleo hasa miradi ya mpango wa maendeleo wa kupambana na UVIKO – 19 katika sekta ya elimu na afya kwa kutumia utaratibu wa “force account” uliotumia muda mfupi wa utekelezaji lakini pia kupunguza gharama za ujenzi kwa kiasi kikubwa.
- Kuboresha utoaji wa huduma za jamii kwa kujenga miundombinu (vyumba vya madarasa na samani zake, majengo katika vituo vya kutolea huduma za afya, matundu ya vyoo na mifumo ya maji safi na maji taka).
- Ununuzi wa dawa na vifaa tiba katika Hospitali, Vituo vya Afya na Zahanati kwa kutumia fedha za mfuko wa pamoja (Basket Fund), Papo kwa Papo, Mfuko wa Afya ya Jamii (CHF) na Bima ya Afya ya Taifa (NHIF)
- Uimarishaji wa huduma za chanjo kwa watoto chini miaka 5 pamoja na chanjo ya UVIKO 19
- Watumishi wamelipwa malimbikizo ya mishahara, madeni mbalimbali pamoja na kupandishwa vyeo na madaraja.
- Mapokezi ya ajira mpya katika idara za Elimu Msingi, Sekondari na idara ya Afya.
- Kupokea idhini ya vibali vya ajira mbadala kwa lengo la kujaza nafasi zilizoachwa wazi na watumishi ambao wamestaafu, kufariki, kuacha kazi na kufukuzwa kazi.

### 2.5.2 Changamoto

- Upungufu wa watumishi katika ngazi ya mkoa na halmashauri hali inayopelekea kuzorota kwa utoaji huduma hasa kada za watendaji wa vijiji, wahasibu, madereva, wakaguzi wa ndani, maafisa uvuvi, sheria, maafisa tawala, maendeleo ya jamii na wataalam wa mifugo.
- Huduma hafifu za mawasiliano katika maeneo ya mipakani hasa Wilaya ya Kyerwa, Karagwe, Missenyi, Ngara na Muleba hali inayosababisha wananchi kukosa mawasiliano imara hivyo kutumia mawasiliano ya simu na vyombo vya habari kutoka nchi jirani, pamoja na kusababisha ugumu wa utendaji kazi kwa mifumo inayotegemea uimara wa mawasiliano.
- Upungufu wa vitendea kazi ngazi ya mkoa na halmashauri mfano; magari, majengo, n.k. upungufu huu unapunguza ufanisi katika ufuatiliaji na utekelezaji wa miradi na utoaji huduma kwa mwananchi.

- Ufinyu wa fedha za kutosha kugharamia miundombinu ukilinganisha na hali halisi na jiografia ya Mkoa wa Kagera, mfano kukamilisha darasa pamoja na kuweka samani kwa shilingi 12,500,000 au kukamilisha Zahanati kwa shilingi 50,000,000 ama kujenga chumba cha vyumba viwili vya madarasa pamoja na kuweka samani na ofisi ya mwalimu katikati kwa gharama ya Shilingi 40,000,000 imebainika hazitoshi kwa mazingira ya mkoa wa Kagera kuwa pembezoni na mbali na viwanda hasa kwa bidhaa za viwandani hii inatokana na gharama kubwa za usafirishaji wa bidhaa, lakini pia mkoa wa Kagera una taadhari ya matetemeko hivyo majengo yote yanayojengwa viwango vyake ni tofauti na majengo yanayojengwa maeneo mengine yasiyokuwa na tahadhari hiyo iliyotolewa na Wakala wa Jiolojia Tanzania (GST) baada ya tetemeko la mwaka 2016. Aidha, gharama za vifaa vya ujenzi zinabadilika kwa kupanda karibu kila mwaka, hali hii imesababisha miradi kutokamilika kwa kiwango kama ilivyokusudiwa.
- Mkoa wa Kagera unapakana na nchi jirani za Uganda, Rwanda, Burundi na Kenya kwa upande wa Ziwa Victoria. Mpaka kati ya Tanzania na nchi hizo una urefu wa km 552.6 na una vipenyo vingi visivyo rasmi (porous), udhibiti wake ni mgumu. Kutokana na hali hiyo, yapo matatizo ya wahamiaji haramu hasa katika Wilaya za Ngara, Kyerwa, Karagwe na Missenyi. Baadhi yao hujihusisha na vitendo vya uhalifu. Mkoa kwa upande wa Ziwa Victoria unapakana na nchi za Uganda na Kenya, mpaka huo wa ziwani ni mrefu na hauna ulinzi wa kutosha kudhibiti vitendo vya uharifu katika ziwa lenye visiwa vipatavyo 48 vilivyo upande wa Mkoa wa Kagera.
- Hali hii umepelekea mkoa kutumia fedha nyingi zinazotolewa kwa ajili ya matumizi mengineyo (OC) katika kuhakikisha hali ya ulinzi na usalama ina imarika na kuwa salama katika maeneo yote ya mkoa. Kiasi kinachotengwa kwa mkoa wa Kagera kwa ajili ya matumizi mengineyo kiongezwe ikiwa ni pamoja na kupatikana kwa vyombo vya usafiri (magari) ili kukabiliana na hali ya usalama katika mkoa huu.
- Kwa kutambua kuwa Mkoa wa Kagera upo takribani kilometa 1,500 kutoka bandari ya Dar es Salaam na kilometa 980 kutoka makao makuu ya nchi, aidha kutokuwa karibu na ofisi, Wizara au taasisi mbalimbali wezeshi. Hali hii imesababisha kuwa na gharama kubwa za usafirishaji wa kufikisha mitambo, malighafi za kuagiza kutoka nje, kusafirisha rasilimali watu hasa wataalam, na kufuata vibali na leseni mbalimbali kwa kuwa taasisi zinazovitoa zipo nje ya Mkoa. Hivyo, gharama hizi kubwa zimechangia sana kuufanya Mkoa wa Kagera kukosa wawekezaji wengi kwenye sekta ya viwanda, biashara pamoja na sekta ya huduma za umma.
- Uongozi wa Mkoa kwa kuzingatia hali hiyo pamoja na ukweli kuwa gharama za uwekezaji na uendeshaji wa viwanda zinatofautiana sana kwa kanda lakini pia Mkoa wetu unapakana na nchi nyinginezo ambazo zinatambua gharama za usafirishaji ni mojawapo ya vikwazo vya kibiashara visivyo vya kikodi (Non-Tariff Trade Barriers - NTBs). Mwezi Oktoba, 2019 liliandaliwa andiko maalum likiwa ni azimio pia la Wiki ya Uwekezaji Kagera iliyofanyika mwezi Agosti, 2019 na kupitishwa na kikao cha Kamati ya Ushauri ya Mkoa cha tarehe 21 Oktoba, 2019, ambalo liliwasilishwa Serikalini kwa ajili ya Mkoa wa Kagera kupewa upendeleo maalum (preferential treatment) kwenye sheria, kanuni na taratibu za kufanya biashara ili kuvutia uwekezaji zaidi kwenye sekta za viwanda na biashara. Tuna imani kwa kufanya hivyo, zipo faida nyingi zitakazopatikana ikiwa ni pamoja na kuongeza kasi ya uwekezaji kwenye viwanda na kwingineko, kuongeza kasi ya uanzishaji biashara mipakani kwa ushindani wa soko la nchini na majirani na kwingineko, kuongeza mzunguko wa uchumi wa Mkoa, kuongeza ajira na pia mapato ya Serikali.

Aidha, upendeleo huu maalum unaweza kutolewa katika mikoa iliyoko pembezoni hasa inayopakana na nchi zenye ushindani mkubwa wa kibiashara na uzalishaji wa viwanda.

### **2.5.3 Mikakati Inayotekelezwa na Kupendekezwa:**

- Kuendelea kuomba ajira mpya ya wataalamu wa fani mbalimbali kupitia mpango na bajeti ya mwaka 2022/2023.
- Kuendelea kutumia rasilimali zilizopo kwa ufanisi na kwa ushirikiano ili kukabiliana na tatizo la vitendea kazi, kama vile vyombo vya usafiri, majengo n.k. Aidha, mkoa na Halmashauri zimeendelea kutenga bajeti kwa ajili ya vitendea kazi.
- Mkoa unapendekeza fedha zinapotolewa kuzingatiwe hali halisi ya maeneo mbalimbali (Mikoa, Wilaya na Halmashauri) na changamoto zake kuliko kutoa fedha kwa viwango sawa nchi nzima bila kujali mahitaji halisi ya eneo husika.
- Kuendelea kuandaa maandiko ili kupata fedha za miradi ya kimkakati ya kuongeza mapato, uwekezaji na huduma. Aidha, Halmashauri zetu zimeendelea pia kutenga sehemu ya mapato yake ya ndani kukamilisha na kuanzisha miradi ya kimkakati.
- Kuimarisha mifumo ya kukusanya na kudhibiti Mapato ya ndani kwa kutumia mifumo ya ki-electroniki, mfano katika bajeti ya mwaka huu hadi sasa mashine za POS zilizonunuliwa (Ngara DC 68, Missenyi DC 19 na Muleba DC 83).
- Kubuni na kuazisha vyanzo vipya vya mapato ya ndani.
- Mkoa kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais - Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Wizara ya Ujenzi pamoja na Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa umekuwa ukiomba katika bajeti za kila mwaka kutengwa fedha kwa ajili ya ujenzi wa barabara za mipakani (security roads) na uimarishaji wa usalama katika ziwa Viktoria.
- Mkoa, ofisi ya Rais TAMISEMI na Wizara ya Mawasiliano kuendelea kushirikiana katika kuhakikisha huduma za mawasiliano zinaboreshwa hasa maeneo ya mipakani.

## SURA YA TATU

### MAKADIRIO YA OFISI YA MKUU WA MKOA NA HALMASHAURI KWA WA MWAKA WA FEDHA 2022/23

#### 3.1 Vipaumbele vya Ofisi ya Mkuu wa Mkoa

Katika mwaka wa fedha 2022/23, Ofisi ya Mkoa imepanga kutekeleza majukumu yake kwa kuzingatia vipaumbele vifuatavyo:

Vipaumbele	Changamoto	Mapendekezo Ya Kutatua Changamoto
<p><b>Kuimarisha Ulinzi na Usalama:</b> Kudumisha ulinzi na usalama katika Mkoa kwa kuwezesha kamati za ulinzi na usalama katika ngazi zote kutekeleza majukumu yake kikamilifu.</p>	<p>Uchache wa rasilimali hasa fedha na vyombo vya usafiri kwa ajili ya usimamizi na ufuatiliaji wa masuala na matukio mbalimbali ya ulinzi na usalama hasa maeneo ya mipakani</p>	<p>Kuongezewa bajeti ya matumizi mengineyo (OC) Sekretarieti ya Mkoa na Ofisi za Mkuu wa Wilaya pamoja na upatikanaji wa vyombo vya usafiri.</p>
<p><b>Kujenga, Kurabati Majengo ya Serikali:</b></p> <ul style="list-style-type: none"> <li>• Kukamilisha ujenzi nyumba ya Mkuu wa Mkoa Kagera.</li> <li>• Kujenga ofisi mpya ya Mkuu wa Wilaya Karagwe, kujenga uzio, landscaping pamoja na kukarabati ofisi ya Mkuu wa Wilaya Misenyi</li> <li>• Kukarabati Ikulu ndogo Bukoba na kukamilisha ujenzi wa ofisi ya Tarafa Murusagamba.</li> </ul>	<p>Ukosefu wa mazingira mazuri ya kufanyia kazi (ofisi, nyumba za kuishi za viongozi).</p>	<p>Kuendelea kutenga fedha kila mwaka katika bajeti kwa ajili ya ujenzi na ukarabati wa ofisi za Serikali na nyumba za kuishi.</p>
<p><b>Upatikanaji wa Vitendea kazi:</b> Upatikanaji wa magari 2 kwa ajili ya usimamizi na ufuatiliaji wa miradi ya maendeleo katika Mkoa</p>	<p>Uchache wa rasilimali hasa fedha na vyombo vya usafiri kwa ajili ya usimamizi na ufuatiliaji wa miradi.</p>	<p>Upatikanaji wa magari angalau 2 kwa kuanzia kwa ajili ya usimamizi na ufuatiliaji miradi ya maendeleo</p>

### 3.2 Vipaumbele vya Halmashauri zote

Eneo	Sekta	Vipaumbele	Changamoto	Mapendekezo ya Kutatua Changamoto
Mamlaka za Serikali za Mitaa Mkoani	Utawala	<p><b>Kujenga, Kurabati Majengo ya Serikali na Samani:</b> Ujenzi, ukarabati na ununuzi wa samani kwa ajili ya majengo ya utawala na nyumba za viongozi wa Halmashari, Ofisi za Kata na Mitaa/Vijiji. Kipaumbele kikiwa kukamilisha miradi inayoendelea kabla ya kuanza miradi mipya ikiwemo ukamilishaji majengo ya utawala kwa Halmashauri za Wilaya za Kyerwa na Bukoba DC pamoja na kukarabati majengo ya utawala katika Halmashauri za Ngara, Biharamulo na Karagwe</p>	Ukosefu wa mazingira mazuri ya kufanyia kazi (ofisi, nyumba za kuishi za viongozi).	Kuendelea kutenga fedha kila mwaka katika bajeti kwa ajili ya ujenzi na ukarabati wa ofisi za Serikali na nyumba za kuishi.
		<p><b>Kuajiri Watumishi:</b> Kuendelea kuomba vibali vya ajira kwenye sekta ya zenye upungufu mkubwa wa watumishi katika Mamlaza za Serikali za Mitaa Mkoani (Wahandisi Ujenzi - <b>95%</b>, Watumishi wa Afya - <b>60%</b>, Maafisa Ushirika - <b>75%</b>, Madereva, Walimu wa Sayansi - <b>48%</b> na Hisabati - <b>60%</b> katika shule za Sekondari na Walimu wa Shule za Msingi pamoja na kuwapa pandisha vyeo watumishi (promotions) wanaostahili kupanda</p>	Upungufu wa watumishi hasa idara za ujenzi, afya, ushirika, madereva, walimu. Aidha kuendelea kuwepo watumishi wengi wanaostahili kupandishwa vyeo (promotions) lakini hawajapandishwa kufuatia hali ya bajeti mishahara kutoruhusu.	Serikali kutenga nafasi za ajira na kutoa vibali vya kuajiri katika idara hizo



Eneo	Sekta	Vipaumbele	Changamoto	Mapendekezo ya Kutatua Changamoto
	Elimu	<p><b>Kuongeza Kiwango cha Ufaulu:</b> Kuongeza kiwango cha ufaulu kwa darasa la VII kutoka <b>88.28%</b> mwaka 2020 hadi <b>98%</b> mwaka 2023; kidato cha sita kuondoa ufaulu wa daraja la sifuri na daraja la nne ifikapo mwaka 2023 ili mkoa ubaki na ufaulu wa daraja la <b>I, II</b> na <b>III</b> pekee. Haya yatafanyika kwa kuboresha maslahi ya walimu (madai yao, likizo, n.k); upatikanaji wa vitendea kazi kama vifaa vya kusomea na kufundishia pamoja na kuimarisha ufuatiliaji na usimamizi wa elimu katika ngazi zote.</p>	Kutotimiza maslahi na mahitaji mbalimbali ya walimu, aidha uchache wa vitendea kazi pamoja na vifaa vya kufundishia na kujifunza kutokana na upungufu wa rasilimali fedha katika bajeti kugharamikia haya yote	Kuendelea kutengewa rasilimali fedha za kutosha katika bajeti za kila mwaka kulingana na mahitaji halisi ya msingi yanayokuwepo
		<p><b>Kupunguza Upungufu wa Miundombinu na Samani:</b> Kuendelea kujenga na kukamilisha miundombinu ya shule za sekondari na msingi ili kukabiliana upungufu wa vyumba vya madarasa (msingi <b>56%</b>, sekondari <b>24%</b>); madawati <b>17%</b>; viti <b>15%</b> na meza <b>9%</b>; nyumba za walimu (msingi <b>87%</b>, sekondari <b>82%</b>) na matundu ya vyoo (msingi <b>64%</b>, sekondari <b>46%</b>); maabara za sayansi <b>44%</b>; shule mpya (msingi <b>32</b>, sekondari <b>16</b> na kidato cha tano na sita <b>8</b>) kwa kushirikiana na wananchi, wadau wa maendeleo na Serikali.</p>	Upungufu mkubwa wa miundombinu wezeshi kwa ajili ya kujifunza na kufundishia hali inayopelekea kushusha kiwango cha utoaji elimu na taaluma kwa ujumla	Kuongeza kiwango cha fedha zina-zotolewa kwa ajili ya ujenzi wa miundombinu na samani kwa shule za msingi na sekondari.

Eneo	Sekta	Vipaumbele	Changamoto	Mapendekezo ya Kutatua Changamoto
	Afyā	<p><b>Kuboresha mazingira ya kutolea huduma za afya:</b> Kwa sasa upungufu wa zahanati ni sawa na <b>58%</b> hivyo kipaumbele ni kujenga na kuboresha zahanati <b>30</b>; vituo vya afya upungufu ni <b>81%</b> hivyo kipaumbele ni kujenga vituo vya afya vipya <b>16</b>, aidha kujenga hospitali mpya <b>2</b> za Ngara DC na Muleba DC pamoja na kukamilisha ujenzi, upatikanaji vifaa tiba na watumishi katika hospitali <b>6</b> (Bukoba DC, Karagwe DC, Kyerwa DC, Biharamulo DC, Bukoba MC na Missenyi DC). Upatikanaji wa magari ya wagonjwa <b>16</b></p>	Baadhi ya maeneo kuwa mbali na huduma za afya hali inayosababisha vifo na wananchi kukosa huduma kwa wakati, aidha uwezo mdogo wa halmashauri (mapato ya ndani) kuweza kujenga na kuboresha vituo vya huduma vinavyohitajika	Serikali kuendelea kutenga fedha hasa za tozo ya miamala ya simu na wadau mbalimbali kupunguza au kumaliza upungufu wa vituo vya kutolea huduma za afya
		<p><b>Kupunguza kiwango cha udumavu (Kuboresha lishe):</b> Kuendelea kutenga <b>Tshs 1,000</b> kwa kila mtoto mwenye umri chini ya miaka <b>5</b> ili kupunguza kiwango cha udumavu katika Mkoa kutoka <b>39.8</b> mwaka <b>2018</b> hadi <b>15%</b> mwaka <b>2023</b></p>	Kutofikiwa kwa malengo ya ukusanyaji mapato ya ndani ya Halmashauri pamoja na fedha za wadau kutoletwa kama ilivyo ahidiwa wakati wa upanogaji bajeti kunaathiri kutenga fedha katika eneo hili	Serikali itenge pia fedha za ndani za maendeleo za kuto-sha, angalau Tshs 1,000 kwa kila mtoto chini ya miaka 5 ili kuweza kutatua tatizo hili

Eneo	Sekta	Vipaumbele	Changamoto	Mapendekezo ya Kutatua Changamoto
	Kilimo	<p><b>Kuongeza uzalishaji wa Mazao ya Biashara na Chakula:</b>  Mazao ya biashara kulima jumla ya <b>hekta 67,934</b> na kuzalisha jumla ya <b>tani 115,885</b> za mazao mbalimbali kama ifuatavyo (Kahawa tani 100,000; pamba tani 9,525; chai tani 6,290 na tumbaku tani 70) katika misimu yote miwili ya mwaka 2022/2023.</p> <p>Aidha, kwa mazao ya chakula kipaumbele ni kulingana jumla ya <b>hekta 628,708</b> na kuzalisha jumla ya <b>tani 4,241,361</b> za mazao mbalimbali kama ifuatavyo (ndizi tani 2,535,574; nafaka tani 329,960; mazao ya mizizi tani 1,244,951 na mazao ya mikunde tani 130,876) katika misimu yote miwili ya mwaka 2022/2023.</p>	<p>Matumizi duni ya pembejeo na zana za kilimo, uhaba wa maafisa ugani na magonjwa hatari ya mimea kama vile mnyauko bakteria au unyanjano kwa migomba (zao kuu la chakula), mnyauko fuzari kwa kahawa (zao kuu la biashara) pamoja na batobato na michirizi ya kahawa kwa mihogo.</p>	<p>Kupatikana kwa rasili-mali za kutosha ili: -</p> <ul style="list-style-type: none"> <li>• Kuhamasishawanchi kushiriki katika shughuli za kilimo hasa mazao ya kimkakati.</li> <li>• Kusambaza mbegu bora.</li> <li>• Kuboresha huduma za ugani.</li> <li>• Kuimarisha masoko na bei</li> <li>• Kuwa na ushirika imara hasa katika zao la kahawa</li> </ul>

Eneo	Sekta	Vipaumbele	Changamoto	Mapendekezo ya Kutatua Changamoto
	Mifugo	<p><b>Ufugaji wa Kisasa na Wenye Tija:</b>  Kuboresha ufugaji kuwa wa kisasa na wenye tija kwa kuchakata/kusarifu bidhaa za mifugo kwa ajili ya mahitaji ya ndani, ikiwemo ya lische bora, na usafirishaji nje ili kuwawezesha wananchi kunufaika na ukuaji wa sekta hiyo. Katika kufikia vipaumbele hicho Mkoa utakeleza yafuatayo:</p> <ul style="list-style-type: none"> <li>• Kuimarisha huduma za ugani katika Kata na Vijiji</li> <li>• Kuboresha afya ya mifugo (kinga, chanjo na tiba)</li> <li>• Kuongeza uzalishaji wa mazao yatoakanayo na mifugo</li> <li>• Kuimarisha huduma za maji, malisho na vya-kula vya mifugo</li> </ul>	<ul style="list-style-type: none"> <li>• Ufugaji bado ni wa kisasi wa ng'ombe aina ya ankole ambao uzalishaji wake wa nyama na maziwa ni duni.</li> <li>• Upungufu wa miundombinu ya mifugo (majosho, mabwawa)</li> <li>• Magonjwa ya mifugo</li> </ul>	<ul style="list-style-type: none"> <li>• Kuajiri maafisa ugani ili kila Kata na Kijiji kifikiwe na mtaalam.</li> <li>• Kuendelea kutenga, kupima na kumiliki-sha maeneo ya ufugaji kwa wafugaji.</li> <li>• Kuhakikisha mifugoyote Mkoani inapatiwa chanjo na dawa za mifugo.</li> <li>• Kuhamasisha sekta binafsi kujenga vinda wanda vya kusindika mazao ya mifugo ili kuongezathamani.</li> <li>• Kuongeza malambo na mabwawa ya maji ya mifugo.</li> </ul>

Eneo	Sekta	Vipaumbele	Changamoto	Mapendekezo ya Kutatua Changamoto
	Uwezeshaji Wanchi kiuchumi	<p><b>Kuwezesha Makundi Maalum Kiuchumi:</b></p> <ul style="list-style-type: none"> <li>• Kuwezesha utoaji wa elimu kwa wajasiliamali ili waweze kuibua miradi ya kiuchumi na kusi-mamia utekelezaji wa sheria ya utoaji mikopo isiyokuwa na riba kwa vikundi vya wanawake, vijana na wenye ulemavu kupitia asimilia 10 ya mapato halisi ya ndani ya Halmashauri.</li> <li>• Kutoa ruzuku kwa kaya masikini kupitia mpango wa jamii wa kunusuru kaya maskini.</li> <li>• Kuendelea kuwatambua wajasiliami wadogo (machinga) na kuwatafutia maeneo sahihi ya kufanyia biashara zao bila kusumbuliwa.</li> </ul>		
	Uchumi, Uwekezaji na Uzalishaji mali	<p><b>Kuboresha mazingira ya Uwekezaji na Biashara:</b></p> <ul style="list-style-type: none"> <li>• Kuibua na kutekeleza miradi ya kimkakati na uwekezaji katika Halmashauri kama stendi za mabasi, maegesho ya magari makubwa na vitega uchumi mbalimbali.</li> <li>• Kuimarisha ukusanyaji wa mapato ya ndani ya Halmashauri ambapo zaidi ya asilimia 40 itaelekezwa kutekeleza miradi ya maendeleo.</li> <li>• Kuainisha fursa mbalimbali katika mkoa na kuhamasisha na kuwezesha sekta binafsi kuwekeza na kufanya biashara.</li> </ul>		<ul style="list-style-type: none"> <li>• Kuupa mkoa wa kagera na mikoa ya pembezoni hasa inayopakana na nchi jirani zenye ushindani mkubwa wa kibashara upendeleo maalum wa kisera katika uwekezaji na biashara.</li> <li>• Serikali kuu kuendelea ku-saidia Halmashauri kupata fedha za utekelezaji wa miradi ya kimkakati (alternative project financing – APF).</li> </ul>

Eneo	Sekta	Vipaumbele	Changamoto	Mapendekezo ya Kutatua Changamoto
	Mipango, ufuatiliaji na Takwimu	<p><b>Usimamizi na Uratibu wa Miradi:</b></p> <ul style="list-style-type: none"> <li>• Kutoa kipaumbele kwa miradi ya ukamilishaji (viporo) hasa maboma ya shule, vituo vya huduma za afya, majengo ya utawala na makazi ya viongozi.</li> <li>• Upatikanaji wa vyombo vya usafiri (magari) kwa ajili ya usimamizi na ufuatiliaji wa miradi ya maendeleo inayotekelezwa katika Kata, Vijiji na Vituo vya huduma (shule na afya).</li> </ul>	<ul style="list-style-type: none"> <li>• Uwepo wa maboma mengi yaliyoanzishwa na nguvu za wananchi, na miradi mingine iliyoanzishwa na Serikali lakini haikukamilika kwa kukosa fedha.</li> <li>• Fedha nyingi zinapelekwa moja kwa moja katika shule na vituo vya kutolea huduma za afya na miradi inayotekelezwa ngazi za Kata na Vijiji kukosa usimamizi mzuri kwasababu ya kukosa usafiri wa kufika katika maeneo hayo ya miradi.</li> </ul>	<p><b>Mapendekezo ya Kutatua Changamoto</b></p> <ul style="list-style-type: none"> <li>• Serikali kuendelea kutenga fedha kwa ajili ya ukamilishaji miradi viporo na maboma yaliyopo na kuanzishwa na wananchi.</li> <li>• Serikali kutenga fedha kwa ajili ya ununuzi wa magari ya usimamizi na ufuatiliaji wa miradi</li> </ul>
	Uendelezaji Miji na Vijiji	Kuboredha huduma za jamii kwa kusimamia na kuratibu uendelezaji wa Ardhi na Makazi ikiwa ni pamoja na kuanzisha miradi ya kupanga, kupima na kumilikisha Ardhi, kurasimisha Ardhi zinazomilikiwa kimila na makazi yasiyo rasmi kwenye miji ili kuwezesha wamiliki wa Ardhi kunufaika na kuchangia maendeleo, Kuanda mipango ya makazi kwenye maeneo yanayokuwa kwa kasi na Kuendelea kuchochea utunzwaji wa misitu kwa kusimamia sheria, kanuni na taratibu.		

### 3.3 Maduhuli na Mapato ya Ndani ya Halmashauri

Mkoa umekisia makusanyo ya **Tshs. 29,407,810,000.00** kutoka kwenye vyanzo vyake. Kati yake **Tshs. 8,960,000.00** ni maduhuli ya Sekretarieti ya Mkoa na **Tshs. 29,398,950,000.00** ni makusanyo ya mapato ya ndani ya Halmashauri.

Makisio ya makusanyo ya Halmashauri kwa ujumla yameongezeka kwa asilimia **14** ikilinganishwa na kiasi kilichoidhinishwa mwaka huu 2021/2022 (**Tshs. 25,701,479,000.00**).

**Jedwali 11 (a): Makadirio ya Maduhuli na Mapato ya Ndani ya Halmashauri Mwaka wa Fedha 2022/23**

Ofisi/Taasisi	Bajeti ya Mwaka 2021/22	Bajeti 2022/23	Ongezeko/ Upungufu	Asilimia ya Ongezeko	Maelezo ya ongezeko au pungufu kwa Makusanyo
Ofisi ya Mkuu wa Mkoa	8,860,000.00	8,860,000.00	0	0	
Biharamulo DC	2,664,937,000.00	2,931,500,000.00	266,563,000.00	10	Ongezeko hilo limetokana na ongezeko la makisio ya mazao mchanganyiko na kuongezwa kwa chanzo cha mapato ya CHANJO (CBPP)
Bukoba DC	1,863,237,000.00	2,080,500,000.00	217,263,000.00	12	Hii imetokana na ongezeko la mwenendowa makusanyo ya vyanzovyada ya maegesho, ushuru wa soko na ushuru wa huduma.
Bukoba MC	3,200,132,000.00	3,520,000,000.00	319,868,000.00	10	ongezeko la mwenendo wa makusanyo ya vyanzo vya ada za leseni za biashara na ushuru wa huduma
Karagwe DC	3,325,510,000.00	3,807,992,000.00	482,482,000.00	15	Kuongeza uthibiti kwa kushirikisha waten-daji wa Kata na Vijiji
Kyerwa DC	2,653,439,000.00	2,919,400,000.00	265,961,000.00	10	Kuongezeka kwa makadirio ya uzalishaji wa zao la kahawa
Missenyi DC	3,669,029,000.00	4,035,900,000.00	366,871,000.00	10	Utafiti wa vyanzo vya mapato ya ndani umefanyika na kubaini mapungufu na kuboresha ukusanyaji.
Ngara DC	2,563,895,000.00	3,766,558,000.00	1,202,663,000.00	47	Mwelekeo wa ukusanyaji kwa miaka 3 mfululizo umeonesha mafanikio yanayotokana udhibiti wa uvujaji wa mapato
Muleba DC	5,761,300,000.00	6,337,100,000.00	575,800,000.00	10	
<b>Jumla Halmashauri</b>	<b>25,701,479,000.00</b>	<b>29,398,950,000.00</b>	<b>3,697,471,000.00</b>	<b>14</b>	
<b>Jumla Kuu</b>	<b>25,710,339,000.00</b>	<b>29,407,810,000.00</b>	<b>3,697,471,000.00</b>	<b>14</b>	



### 3.4 Makisio ya Mapato Ndani lindwa, yasiyolindwa, Makisio ya Matumizi ya Kawaida, na Maendeleo

Jedwali Na.11 (b) Makisio kwa Mgawanyo wa makisio yasiyolindwa, Lindwa, Matumizi ya Kawaida na Maendeleo Mwaka 2022/23.

Halmashauri	Jumla ya Makisio 2022/23	Makisio Lindwa 2022/23	Makiso yasiyo-lindwa	Matumizi ya Kawaida	Matumizi ya Maendeleo	Maelezo kama 40 au 60 ya Maendeleo
Bukoba DC	2,080,500,000	475,000,000	1,605,500,000	1,438,300,000	642,200,000	40%
Biharamulo DC	2,931,500,000	1,048,300,000	1,883,200,000	2,178,220,000	753,280,000	40%
Karagwe DC	3,807,992,000	754,605,000	3,053,386,000	2,586,637,000	1,221,355,000	40%
Muleba DC	6,337,100,000	1,071,400,000	5,265,700,000	4,230,820,000	2,106,280,000	40%
